Tanzania

# Kilimo cha Biashara kwa wakulima Wadogo Zanzibar (CASH)

Kuwatambua Wahisani:
VSO Tanzania – Meneja mradi
UWAMWIMA – Chama cha Wakulima wa Mboga
UWZ – Chama cha watu wenye Ulemavu
WEDTF – Mfuko wa Udhamini wa Maendeleo ya Ujasiriamali wa Wanawake
KATI – Taasisi ya Mafunzo ya Kilimo Kizimbani

Mradi wa Kilimo cha Biashara kwa Wakulima Wadogo (CASH) una lengo la kuwawezesha wakulima wadogo wadogo kushiriki katika soko na kuboresha kilimo toka shughuli ya kujikimu, kuwa biashara yenye kutoa faida. Mradi huu unafadhiliwa na Cordaid na Accenture, na unatekelezwa na shirika la VSO kwa kushirikiana na UWAMWIMA, UWZ, KATI na WEDTF. Mradi huu unafanya kazi katika mfumo wa Programu ya Riziki Salama ya VSO Tanzania ambayo inalenga katika kuboresha mnyororo wa thamani ya kilimo kwa kuhakikisha kuwa wakulima wadogo wadogo wanapata rasilimali za uzalishaji (ardhi, mikopo midogo), teknolojia sahihi (umwagiliaji, mbegu), utekelezaji wa kilimo kizuri na mahusiano ya soko.

**Kwa nini? Kusaidia wakulima wadogo wa Zanzibar katika Kilimo cha Biashara.**

Zanzibar ni kisiwa kidogo c henye wakazi zaidi ya milioni moja, ambao wengi wao ni wakulima wadogo wadogo. Utalii imekuwa sekta kuu katika miaka 20 iliyopita, lakini

wakulima wa Zanzibar hawanufaiki na watalii wanaotembelea kisiwa hicho wanaokadiriwa kuwa milioni 1 kwa mwaka, sehemu kubwa ya Zanzibar ambayo imekua maarufu kwa mashamba yake ya viungo hailimwi tena na asilimia 80 ya mboga mboga na matunda yanayotolewa kwa sekta ya hoteli hayatoki kisiwani humo.

**Nini? Malengo ya mradi wa CASH. Mradi wa CASH huwasaidia wakulima wadogo katika:**

A. Kuboresha tija na ubora kwa vikundi kupata huduma za uzalishaji, upanuzi na mafunzo na kupunguza gharama za uzalishaji kwa kununua idadi kubwa ya vifaa (vikiwemo mbegu, mbolea na vifaa vingine).
B. Kuboresha uwezo wa mkulima kushiriki katika masoko yenye faida kubwa
C. Kuanzisha mzunguko wa fedha kama njia ya kugharamia huduma za matumizi ya kawaida na vifaa.

Wakati wa utekelezaji wa mradi huu, kumekuwa na ongezeko la idadi ya Wazanzibari wanaotumia mbinu bora za uzalishaji na, idadi ya wanawake kushiriki katika ngazi zote za mnyororo wa thamani ya kilimo ikiwa ni pamoja na masoko ya bidhaa kwa hoteli za kitalii. Utafiti uliofanywa na VSO Tanzania katika kutathimini mafanikio ya maradi wake wa kutengeneza masoko kwa ajili ya waitu masikini (MMW4P) umeonesha ongezeko la kipato cha zaida ya asilimia 50.

Kilimo cha Biashara kwa wakulima Wadogo Zanzibar (CASH)

**Walengwa**

- Vikundi 14 vya wakulima kutoka Chutama, Kivunge, Mchangani, Tunduni, Chechele, Chuini, Kiboje, Mahonda, Mbuzini, Mchangani, Mfenesini, Munduli, Nyamanzi na Paje vinapewa mbinu bora za kilimo na huduma za mikopo midogo midogo.
- Wanajamii 256 ikiwa ni pamoja na wanawake, vijana, watu wenye ulemavu, watu wanaoishi na VVU na UKIMWI ambao asilimia 21 ni wanaume na asilimia 78 wanawake wanapata mafunzo ya mbinu bora za kilimo, pembejeo na misaada ya pesa za vifaa na mafunzo ya masoko.
- Wajasiriamali 400 katika fani ya usindikaji wa chakula na nyongeza ya thamani ya mboga wanaunganishwa na soko kupitia mawakala.
- Mawakala 10 wa masoko ya kilimo wanaunganishwa na wakulima wa ndani na mazao yao.
- Wafanyakazi wa ugani 4 kutoka Wizara ya Kilimo na Maliasili wanapata msaada wa kiufundi.

**Shughuli Zinazotolewa**

A. Kufanya Uchumi wa Kilimo na Mafunzo ya Stadi za Ujasiriamali
B. Kuanzisha Shule za Fani ya Mkulima
C. Ziara ya Mafunzo ya Wakulima
D. Kuunganisha na wauzaji wa pembejeo, masoko ya ndani na utalii
E. Uhamasishaji wa Ugani na Vikao vya Mipango
F. Ziara ya Tathimini ya Ugani na Mchakato wa Mafunzo
G. Nyongeza ya thamani
H. Utafiti wa Masoko
I. Huduma za mikopo Midogodogo

**Mchango wa Kiufundi wa VSO**

VSO hutoa msaada wa kiufundi na kitaalamu kama ifuatavyo:

- Mshauri wa Maendeleo ya Mikopo Midogo Midogo
- Wataalamu wa mnyororo wa thamani na maendeleo ya biashara
- Wataalamu wa kilimo na masoko
- Mshauri wa utamaduni wa ufugaji wa samaki
- Mchanganuzi wa dhamana ya chakula na lishe
- Mshauri Mhandisi wa kilimo

**Muda wa Mradi**

Januari 2012 hadi Desemba 2013

**Programu ya VSO ya Riziki Salama**

VSO ni shirika la maendeleo la kimataifa linalofanya kazi kupita wataalamu wa kujitolea katika kupambana na umaskini. Tumekuwa tukifanya kazi nchini Tanzania kwa zaidi ya miaka 52 kwa ushirikiano wa karibu na taasisi mbalimbali za Serikali na wadau wa vyama vya kiraia. Tumechangia hasa mafanikio ya malengo ya Wizara ya Kilimo katika utoaji wa huduma bora za kilimo na dhamana ya chakula, kujenga uwezo wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa na kuiwezesha sekta binafsi kuchangia kikamilifu katika uzalishaji endelevu wa kilimo, chakula na maendeleo ya lishe katika mikoa mbalimbali nchini Tanzania.

**Programu hii imeundwa kufikia matokeo muhimu yafuatayo:**

- Taasisi za mafunzo ya Ufundi Stadi kuongeza viwango vyao kulingana na viwango vinavyotambulika kimataifa na mahitaji ya soko.
- Wakulima wadogo wanapata rasilimali za uzalishaji (ardhi, mikopo midogo), teknolojia sahihi (umwagiliaji, mbegu), kutekeleza kilimo bora na mahusiano ya soko.
- Mazingira ya kibiashara yanafaa zaidi kwa maendeleo ya sekta binafsi, hasa SME.

Kwa mawasiliano zaidi wasiliana na
Jean van Weter - jean.vanweter@vsoint.org
Rose Tesha - rose.tesha@vsoint.org
Ofisi: Na. ya Kitalu 997 - Barabara ya Kahama - Msasani; S.L.P. 6297 Dar es Salaam
Simu: +255 22 2600072
**www.vsointernational.org**

VSO Tanzania accenture Cordaid